# TOLEO LA TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA KWA WANAWAKE NA WATOTO -ZANZIBAR, OKTOBA MWAKA 2021

**Na: 10**

*Office of Chief Government Statistician*

*P.O. Box 2321, Zanzibar*
Telephone +255242231869
Email: zanstat@ocgs.go.com
Website: http://www.ocgs.go.tz

*UN Women Office*
392Toure Drive, Masaki
Dar es Salaam
Tanzania

*Police Headquarter Zanzibar*

P.O.Box 237, PHQ Zanzibar
Fax No: 0242231367
Email:cidhqznz@gmail.com

## Utangulizi

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu kwa kushirikiana na Shirika la Wanawake la Umoja wa Mataifa wameandaa utaratibu ambao utawezesha ofisi kutekeleza majukumu yake iliyojipangia kuimarisha takwimu za jinsia. Miongoni mwa takwimu hizo ni kukuksanya takwimu za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kjinsia.

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6).


## Lengo

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera, na watoa maamuzi.

## Matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia

Jumla ya matukio 107 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Oktoba, 2021. Kulikuwa na waathirika 107 ambao waathirika Wanawake ni 13 (asilimia 12.1) na watoto ni 94 sawa na asilimia 87.9, miongoni mwao wasichana ni 81 (asilimia 86.2) na wavulana ni 13 (asilimia 13.8).


**Kielelezo 1.1: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto, Oktoba 2021**




**Chanzo: Makao** makuu ya Polisi –Zanzibar

Wilaya ya Magharibi "A" imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyegine (matukio 21), zikifuatia wilaya ya Mjini (matukio 16) na wilaya ya Wete (matukio 15). Wilaya ya Kaskazini "A" imeripotiwa kuwa na idadi ndogo zaidi ya matukio kuliko wilaya zote (tukio moja (1)).

**Kielelezo 1.2: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto kwa Wilaya, Oktoba 2021**




**Chanzo:** Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Mlinganisho wa idadi ya matukio kwa mwezi imeongezeka kwa asilimia 18.9 kutoka matukio 90 kwa mwezi wa Septemba, 2021 hadi 107 mwezi wa Oktoba, 2021. Aidha wilaya Magharibi "B" iliongoza kwa idadi kubwa ya matukio kwa mwezi Septemba (matukio 21), ambapo wilaya ya Magharibi "A" imeongoza kwa mwezi wa Oktoba 2021(matukio 21). Wilaya ya Micheweni imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio kwa mwezi wa Septemba 2021 (matukio matatu (3)) ambapo Kaskazini "A" hakukuripotiwa tukio lolote ambapo wilaya ya Kaskazini "A" iliripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio kwa mwezi wa Oktoba 2021 (tukio moja (1)).

**Jadweli 1.1: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Mwezi Septemba 2021 na Oktoba 2021**

| Wilaya | Idadi ya matukio | | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Septemba 2021 | Oktoba 2021 | Septemba 2021 | Oktoba 2021 | Septemba 2021 | Oktoba 2021 | Septemba 2021 | Oktoba 2021 | Septemba 2021 | Oktoba 2021 | Septemba 2021 | Oktoba 2021 | Septemba 2021 | Oktoba 2021 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 5 | 7 | 4 | 6 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 9 | 11 | 6 | 9 | 0 | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 5 | 2 | 3 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 13 | 16 | 4 | 9 | 5 | 1 | 0 | 1 | 1 | 1 | 2 | 2 | 1 | 2 |
| Magharibi 'A' | 11 | 21 | 6 | 7 | 3 | 2 | 0 | 7 | 0 | 1 | 0 | 2 | 2 | 2 |
| Magharibi 'B' | 21 | 12 | 12 | 4 | 3 | 1 | 0 | 2 | 1 | 1 | 2 | 0 | 3 | 4 |
| Wete | 9 | 15 | 5 | 1 | 0 | 5 | 0 | 0 | 2 | 2 | 2 | 7 | 0 | 0 |
| Micheweni | 3 | 9 | 3 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Chake | 10 | 10 | 3 | 7 | 1 | 1 | 1 | 0 | 2 | 1 | 3 | 1 | 0 | 0 |
| Mkoani | 4 | 3 | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **90** | **107** | **50** | **54** | **14** | **10** | **3** | **13** | **7** | **8** | **10** | **14** | **6** | **8** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Mlinganisho wa idadi ya matukio kwa mwaka imeongezeka kwa asilimia 3.9 kutoka matukio 103 kwa mwezi wa Oktoba, 2020 hadi 107 mwezi wa Oktoba, 2021. Ambapo Mjini iliongoza kwa idadi kubwa ya matukio kwa mwezi Oktoba, 2020 (matukio 29) na Magharibi "A" imeongoza zaidi kwa idadi ya matukio mwezi wa Oktoba, 2021 (matukio 21).

**Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Mwezi Oktoba 2020 na Oktoba 2021**

| Wilaya | Idadi ya matukio | | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Oktoba 2020 | Oktoba 2021 | Oktoba 2020 | Oktoba 2021 | Oktoba 2020 | Oktoba 2021 | Oktoba 2020 | Oktoba 2021 | Oktoba 2020 | Oktoba 2021 | Oktoba 2020 | Oktoba 2021 | Oktoba 2020 | Oktoba 2021 |
| Kaskazini 'A' | 2 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 9 | 7 | 6 | 6 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 6 | 11 | 1 | 9 | 0 | 0 | 0 | 2 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 2 | 2 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 29 | 16 | 8 | 9 | 10 | 1 | 2 | 1 | 3 | 1 | 1 | 2 | 5 | 2 |
| Magharibi 'A' | 13 | 21 | 8 | 7 | 2 | 2 | 1 | 7 | 0 | 1 | 0 | 2 | 2 | 2 |
| Magharibi 'B' | 19 | 12 | 5 | 4 | 0 | 1 | 0 | 2 | 5 | 1 | 2 | 0 | 7 | 4 |
| Wete | 7 | 15 | 6 | 1 | 1 | 5 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 7 | 0 | 0 |
| Micheweni | 6 | 9 | 4 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 6 | 10 | 5 | 7 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Mkoani | 4 | 3 | 2 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **103** | **107** | **48** | **54** | **15** | **10** | **3** | **13** | **19** | **8** | **4** | **14** | **14** | **8** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Miongoni mwa waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia waliobakwa ni 54, wanawake walikuwa nane (8) na wasichana ni 46, waliolawitiwa ni 10, Kuingiliwa kinyume na maumbile 13 wote ni wasichana, Kutorosha walikuwa nane (8) wote ni wasichana, shambulio la aibu walikuwa 14 (mwanamke mmoja (1) na wasichana walikuwa 13) na shambulio walikuwa nane (8) (wanawake wanne (4), msichana mmoja (1) na wavulana walikuwa watatu (3)).

**Jadweli 1.3: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Oktoba 2021**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 4 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 10 | 8 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 13 | 7 | 1 | 1 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 1 |
| Magharibi 'A' | 20 | 7 | 2 | 7 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 1 |
| Magharibi 'B' | 10 | 4 | 1 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Wete | 14 | 1 | 5 | 0 | 2 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 9 | 6 | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 9 | 6 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **94** | **46** | **10** | **13** | **8** | **0** | **13** | **0** | **1** | **3** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

**Jadweli 1.4: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake kwa Wilaya, Oktoba 2021**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Magharibi 'A' | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Magharibi 'B' | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Wete | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **13** | **8** | **0** | **0** | **1** | **4** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Watoto wenye umri wa miaka 15-17 wameripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio 46 sawa asilimia 48.9 ya matukio yote ya watoto ni zaidi ya robo moja (1) ikifuatiwa na umri wa miaka 11-14 (matukio 26) ukilinganisha miaka mengine ya watoto. Aidha matukio ya kubaka yanaonesha kuwa mengi zaidi katika umri huo.

**Jadweli 1.5: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Oktoba 2021**

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla |
| | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | |
| 0-5 | | 4 | 2 | | | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 8 |
| 6-10 | | 1 | 3 | | | 3 | 0 | 1 | 0 | 6 | 0 | 0 | 14 |
| 11-14 | | 12 | 2 | | | 7 | 0 | 1 | 0 | 4 | 0 | 0 | 26 |
| 15-17 | | 29 | 3 | | | 2 | 0 | 6 | 0 | 2 | 3 | 1 | 46 |
| **Jumla** | | **46** | **10** | | | **13** | **0** | **8** | **0** | **13** | **3** | **1** | **94** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Idadi ya watoto waathirika wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa mwezi wa Oktoba, 2021 imeongezeka kwa asilimia 16.0 (matukio 94) ukilinganisha na mwezi wa Septemba, 2021 (matukio 81). Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika wenye umri wa miaka 15-17 kwa mwezi uliopita imeongezeka kwa asilimia 7.0 kutoka matukio 43 kwa mwezi Septemba hadi matukio 46 kwa mwezi wa Oktoba 2021.

**Jadweli 1.6: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Mwezi Septemba 2021 na Oktoba 2021**

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Septemba 2021 | Jumla Oktoba 2021 |
| | Septemba 2021 | Oktoba 2021 | Septemba 2021 | Oktoba 2021 | Septemba 2021 | Oktoba 2021 | Septemba 2021 | Oktoba 2021 | Septemba 2021 | Oktoba 2021 | Septemba 2021 | Oktoba 2021 | | |
| 0-5 | 0 | 4 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 8 |
| 6-10 | 3 | 1 | 4 | 3 | 1 | 3 | 0 | 1 | 4 | 6 | 0 | 0 | 12 | 14 |
| 11-14 | 13 | 12 | 7 | 2 | 1 | 7 | 0 | 1 | 5 | 4 | 0 | 0 | 26 | 26 |
| 15-17 | 28 | 29 | 3 | 3 | 1 | 2 | 6 | 6 | 0 | 2 | 5 | 4 | 43 | 46 |
| **Jumla** | **44** | **46** | **14** | **10** | **3** | **13** | **6** | **8** | **9** | **13** | **5** | **4** | **81** | **94** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika wenye umri wa miaka 15-17 kwa mwaka uliopita imepungua kwa asilimia 16.0 kutoka matukio 55 kwa mwezi wa Oktoba, 2020 hadi matukio 46 kwa mwezi wa Oktoba, 2021. Mwezi wa Oktoba 2020 na Oktoba 2021 umri wa miaka 15-17 ilikuwa na waathirika wengi zaidi kuliko umri mwengine na umri wa 0-5 ilikuwa na waathirika kidogo kwa miezi hiyo.


**Jadweli 1.7: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Mwezi Oktoba 2020 na Oktoba 2021**

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Oktoba 2020 | Jumla Oktoba 2021 |
| | Oktoba 2020 | Oktoba 2021 | Oktoba 2020 | Oktoba 2021 | Oktoba 2020 | Oktoba 2021 | Oktoba 2020 | Oktoba 2021 | Oktoba 2020 | Oktoba 2021 | Oktoba 2020 | Oktoba 2021 | | |
| 0-5 | 0 | 4 | 1 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 8 |
| 6-10 | 5 | 1 | 3 | 3 | 1 | 3 | 1 | 1 | 3 | 6 | 1 | 0 | 14 | 14 |
| 11-14 | 9 | 12 | 2 | 2 | 1 | 7 | 3 | 1 | 0 | 4 | 2 | 0 | 17 | 26 |
| 15-17 | 27 | 29 | 9 | 3 | 1 | 2 | 12 | 6 | 1 | 2 | 5 | 4 | 55 | 46 |
| **Jumla** | **41** | **46** | **15** | **10** | **3** | **13** | **16** | **8** | **4** | **13** | **8** | **4** | **87** | **94** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Matukio 60 kati ya matukio 107 yanaonekana yametokea Nyumbani sawa na asilimia 56.0 na matukio matukio 47 yametokea Sehemu nyengine  sawa na asilimia 44.0.

**Kielelezo 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto na Sehemu Yaliyotokea, Oktoba 2021**




Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Mlinganisho wa matukio yaliyotokezea sehemu nyengine  kwa mwezi yameongezeka kwa asilimia 67.9 kutoka matukio 28 kwa mwezi wa Septemba, 2021 hadi matukio  47 kwa mwezi wa Oktoba, 2021, ambapo matukio yaliyotokea nyumbani yamepungua kwa asilimia 1.6 kutoka matukio 61 kwa mwezi wa Septemba 2020 hadi matukio 60 kwa mwezi wa oktoba 2021.

**Jadweli 1.8: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto na Maeneo yaliyofanyika Matukio, Septemba 2021 na Oktoba 2021**

| Eneo la matukio | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Septemba 2021 | Jumla Oktoba 2021 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Septemba 2021 | Oktoba 2021 | Septemba 2021 | Oktoba 2021 | Septemba 2021 | Oktoba 2021 | Septemba 2021 | Oktoba 2021 | Septemba 2021 | Oktoba 2021 | Septemba 2021 | Oktoba 2021 | | |
| Nyumbani | 33 | 24 | 13 | 4 | 1 | 11 | 3 | 6 | 5 | 7 | 6 | 8 | 61 | 60 |
| Kazini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Skuli/Madrasa | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Sehemu nyengine | 16 | 30 | 1 | 6 | 2 | 2 | 4 | 2 | 5 | 7 | 0 | 0 | 28 | 47 |
| **Jumla** | **50** | **54** | **14** | **10** | **3** | **13** | **7** | **8** | **10** | **14** | **6** | **8** | **90** | **107** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Mlinganisho wa idadi ya matukio yaliyotokea nyumbani kwa mwaka uliopita imepungua kwa asilimia 31.8 kutoka matukio 88 kwa mwezi wa Oktoba, 2020 hadi 60 mwezi wa Oktoba , 2021.

**Jadweli 1.9: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto na Maeneo yaliyofanyika Matukio, Oktoba 2020 na Oktoba 2021**

| Eneo la matukio | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Oktoba 2020 | Jumla Oktoba 2021 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Oktoba 2020 | Oktoba 2021 | Oktoba 2020 | Oktoba 2021 | Oktoba 2020 | Oktoba 2021 | Oktoba 2020 | Oktoba 2021 | Oktoba 2020 | Oktoba 2021 | Oktoba 2020 | Oktoba 2021 | | |
| Nyumbani | 38 | 24 | 15 | 4 | 3 | 11 | 14 | 6 | 4 | 7 | 14 | 8 | 88 | 60 |
| Kazini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Skuli/Madrasa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu nyengine | 10 | 30 | 0 | 6 | 0 | 2 | 5 | 2 | 0 | 7 | 0 | 0 | 15 | 47 |
| **Jumla** | **48** | **54** | **15** | **10** | **3** | **13** | **19** | **8** | **4** | **14** | **14** | **8** | **103** | **107** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Matukio 75 yapo chini ya upelelezi wa Polisi, matukio 17 yapo mahakamani, matukio 13 yapo Ofisi ya Mashtaka, tukio moja (1) limefungwa polisi na tukio moja (1) limetiwa hatiani.


**Jadweli 1.10: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto na Hatua Zilizochukuliwa, Oktoba 2021**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | Waathirika | | | Hatua zilizochukuliwa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Wanawake | Watoto | | Zilizo Mahakamani | Zilizotiwa hatiani | Ziliachiwahuru | Zilizofungwa Polisi | Zilizopelekwa kwa Ofisi ya M' mashtaka | Zilizo chini ya Upelelezi wa Polisi |
| | | | Wasichana | Wavulana | | | | | | |
| Kubaka | 54 | 8 | 46 | | 9 | 1 | 0 | 1 | 9 | 34 |
| Kulawiti | 10 | | | 10 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 8 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 13 | 0 | 13 | | 4 | 0 | 0 | 0 | 3 | 6 |
| Kutorosha | 8 | 0 | 8 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 14 | 1 | 13 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 |
| Shambulio | 8 | 4 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 8 |
| **Jumla** | **107** | **13** | **81** | **13** | **17** | **1** | **0** | **1** | **13** | **75** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi -Zanzibar

Wafanyaji wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia ni jirani walikuwa ni 60 sawa na asilimia 56.1 kati ya wafanyaji wote walioripotiwa, wapita njia walikuwa 47 sawa na asilimia 43.9.

**Kielelezo 1.4: Aina ya Watu Waliofanya Matukio ya Ukatiki na Udhalilishaji wa Kijinsia, Oktoba 2021**




Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

## Kiambatanisho

**Jadweli 1.0: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto na Maeneo yaliyofanyika**

**Matukio, Oktoba 2021**

| Eneo la matukio | Kubaka | | | Kulawiti | | | Kuingilia kinyume na maumbile | | | Kutorosha | | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | | Shambulio | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla |
| Nyumbani | 24 | [redacted] | 24 | [redacted] | 4 | 4 | 11 | [redacted] | 11 | 6 | 0 | 6 | 7 | 0 | 7 | 5 | 3 | 8 |
| Kazini | 0 | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Skuli/Madrasa | 0 | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu nyengine | 30 | [redacted] | 30 | [redacted] | 6 | 6 | 2 | [redacted] | 2 | 2 | 0 | 2 | 7 | 0 | 7 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **54** | [redacted] | **54** | [redacted] | **10** | **10** | **13** | [redacted] | **13** | **8** | **0** | **8** | **14** | **0** | **14** | **5** | **3** | **8** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

**Jadweli 2.0: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Oktoba 2021**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 7 | 6 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 11 | 9 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 16 | 9 | 1 | 1 | 1 | 2 | 2 |
| Magharibi 'A' | 21 | 7 | 2 | 7 | 1 | 2 | 2 |
| Magharibi 'B' | 12 | 4 | 1 | 2 | 1 | 0 | 4 |
| Wete | 15 | 1 | 5 | 0 | 2 | 7 | 0 |
| Micheweni | 9 | 6 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 |
| Chake Chake | 10 | 7 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 |
| Mkoani | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **107** | **54** | **10** | **13** | **8** | **14** | **8** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

**Jadweli 3.0: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto, Mwezi Septemba 2021 na Oktoba 2021**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | | Waathirika | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | |
| | Septemba 2021 | Oktoba 2021 | Septemba 2021 | Oktoba 2021 | Septemba 2021 | Oktoba 2021 | Septemba 2021 | Oktoba 2021 |
| Kubaka | 50 | 54 | 6 | 8 | 44 | 46 | | |
| Kulawiti | 14 | 10 | | | | | 14 | 10 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 3 | 13 | 0 | 0 | 3 | 13 | | |
| Kutorosha | 7 | 8 | 1 | 0 | 6 | 8 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 10 | 14 | 1 | 1 | 7 | 13 | 2 | 0 |
| Shambulio | 6 | 8 | 1 | 4 | 2 | 1 | 3 | 3 |
| **Jumla** | **90** | **107** | **9** | **13** | **62** | **81** | **19** | **13** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi -Zanzibar

**Jadweli 4.0: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto, Mwezi Oktoba 2020 na Oktoba 2021**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | | Waathirika | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | |
| | Oktoba 2020 | Oktoba 2021 | Oktoba 2020 | Oktoba 2021 | Oktoba 2020 | Oktoba 2021 | Oktoba 2020 | Oktoba 2021 |
| Kubaka | 48 | 54 | 7 | 8 | 41 | 46 | | |
| Kulawiti | 15 | 10 | | | | | 15 | 10 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 3 | 13 | 0 | 0 | 3 | 13 | | |
| Kutorosha | 19 | 8 | 3 | 0 | 15 | 8 | 1 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 4 | 14 | 0 | 1 | 4 | 13 | 0 | 0 |
| Shambulio | 14 | 8 | 6 | 4 | 4 | 1 | 4 | 3 |
| **Jumla** | **103** | **107** | **16** | **13** | **67** | **81** | **20** | **13** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

## Zingatia Maelezo

**Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia**

Kitendo chochote au mwenendo wowote, ambao husababisha moja kwa moja kwa mtu, kama mateso ya kimwili, ya kimapenzi au ya kiakili kupitia vitisho, kulazimisha au njia zingine; lengo la kutisha, kuadhibu, kuwadhalilisha, kudhoofisha usalama au kujiheshimu; kutosheleza hamu ya ngono; au kudhoofisha uwezo wa mwili au kiakili wa mtu kwa sababu ya jinsi yake. Kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia, kumpiga mke, unyanyasaji wa kijinsia wa wasichana na wavulana, ukeketaji wa kike, mwanamke kuua watoto wachanga, utoaji mimba, ukahaba wa kulazimishwa , Biashara haramu ya usafirishaji wa wanawake na watoto wa kike na ponografia (uenezaji wa ngono haramu).

Sheria ya Adhabu ya 6/2018 iliongeza adhabu kwa makosa yanayohusiana na maadili kama vile ubakaji, kulawiti, kuingilia kinyume na kimaumbile na shambulio la aibu;

Sheria hii imetungwa mwaka 2018 ambayo imekuja kufuta sheria kama hii ya mwaka 2004. Sheria hii imetungwa pamoja na mambo mengine kuyafanya baadhi ya matendo kuwa makosa ya jinai na kuyawekea adhabu zake endapo mtu yeyote atayatenda matendo hayo na mahkama itamuona ana hatia. Kwenye shehemu ya kumi na tatu (Section thirteen) ya sheria ya adhabu imejumuisha makosa mengi ambayo ni makosa dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto

Sheria ya mwenendo wa Jinai 7/2018 kifungu cha 151 (1) kina vifungu ambavyo haviruhusu utoaji wa dhamana kwa mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kesi zinazohusiana na ukatili na udhalilishaji wa kijinsia, pamoja na kuongezeka kwa hukumu ambazo Mahakama zinaweza kupitisha. Kwa mfano, katika Mahakama ya Mkoa kesi za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kutoka miaka 7 hadi miaka 14 na kwa Mahakama Kuu kutoka miaka 30 hadi kifungo cha maisha.

**Kwa ufafanuzi zaidi tafadhali wasiliana na:**

***Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali***
***Sanduku la barua, 2321***
***Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz***

***Makao Makuu ya Polisi Zanzibar***
***Sanduku la barua, 237, MMP, Zanzibar***
***Barua pepe:cidphqznz@gmail.com***